

**MAHUBIRI KATIKA IBADA YA UDUGU USHARIKA WA HIMMELFAHRT- Munich
PASING TAR: 13.02.2022**

WAZO KUU: „Mchukuliane Mizigo“

SOMO LA MAHUBIRI: Wagalatia 6:2 „Mchukuliane Mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo“.

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na upendo wa Mungu na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nasi sote. Amina!

Sala fupi:.....

Wapendwa Kaka na Dada katika Kristo, ninawasalimu katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo; Bwana Yesu asifiwe! tunayo kila sababu ya kumshukuru Mungu, ambaye ametuwezesha kuadhimisha Ibada hii ya Udugu. Wazo kuu katika Ibada hii ya Udugu mwaka huu 2022 linasema “**Mchukuliane Mizigo**”. Katika Waraka wa Mtume Paulo kwa Wagalatia, “Ni jinsi gani mtu aweze Kuhesabiwa Haki mbele za Mungu” linaonekana ni wazo ambalo limetawala katika waraka huu kwa Wagalatia. Baada ya Mtume Paulo kuhubiri Injili kule Galatia, kwamba mtu anahesabiwa haki kwa imani ya kumwamini Yesu Kristo, wako Walimu wengine ambaeo walienda huko na kueneza Mafundisho na mikazo ya namna nyingine. Mkazo mmojawapo ulikuwa ni kwamba mtu ni lazima ashike Sheria ya Musa, ndipo anaweza kuhesabiwa haki. Kwa lugha nyingine, katika mkazo huu Imani katika Kristo haikuwa na nafasi kubwa sana kwao, bali sheria ya Musa. Katika Mkazo huu, baadhi ya sheria ziliwafanya wakati mwingine kutokuwa na uhusiano mzuri na watu wengine, wakati mwingine waliacha hata kula pamoja na Wakristo wengine wa Mataifa, wakiogopa kuvunja sheria ya Musa.

Kwa hali hii Mtume Paulo alijua kuwa Wakristo wale wa Galatia moja kwa moja walikabiliwa na matatizo au changamoto mbalimbali. Inawezekana walikuwa na changamoto zingine za Kibinadamu, lakini mojawawapo ilikuwa ni changamoto za kiroho, pia matatizo ya uhusiano wa wao kwa wao, walikuwa katika hali ya mashaka, walisahau kwamba Uhusiano wao na Kristo Yesu msingi wake ulikuwa katika kumwamini na hivyo kugeukia Mikazo mingine. Kwa hakika walihitaji kurejeshwa kwenye njia iliyo sahihi ya uhusiano na Mungu. Mstari ambaeo ni somo la Mahubiri leo, Mtume Paulo anawakumbusha namna ya kutatua changamoto za namna hiyo. Anaeleza juu ya **Kuchukuliana Mizigo**. Mizigo ni hali yoyote iliyo ngumu, inaweza kuwa ya kiroho, inaweza kuwa ya kimwili, inaweza kuwa ya kiakili au kihisia. Sote tunajua kwamba ipo Mizigo au Changamoto ambazo unaweza kushughulikia peke yako na zikaisha, lakini changamoto zingine zinahitaji mtu mwingine atusaidie, ndipo ziishe. Ndiyo maana Mtume Paulo anasema: „**Mchukuliane Mizigo na kuitimiza hivyo**

sheria ya Kristo“. Kwamba katika kuchukuliana Mizigo, sheria ya Kristo (siyo ya Musa) inatimizwa. Sheria ya Kristo ni ipi? Hapa tunakumbushwa juu ya Amri kuu ya Upendo (yaani kumpenda Mungu kwa Moyo wako wote na kumpenda jirani yako kama nafsi yako).

Wapendwa kaka na Dada katika Kristo, sisi pia katika maisha tunayoishi tuna Mizigo mbalimbali. Inawezekana inatofautiana tu kwa ukubwa, sura au aina lakini tunayo mizigo. Mizigo hiyo inaweza kuwa ni Magonjwa, Mahusiano mabaya katika Familia, kukatishwa tamaa, kufiwa, Mahusiano mabaya katika eneo la Kazi, matatizo ya kifedha/Umaskini, Majanga ya asili, mzigo wa Majaribu, n.k. Kwa hiyo mstari huu “Mchukuliane Mizigo” unatugusa sisi sote, kwa kila Mkristo lakini pia kama Kanisa la Mungu katika Ulimwengu mzima. Kama vile Askari-jeshi wanavyobeba “mizigo” yao wanavyokwenda vitani, lakini wakati huohuo mmoja wao anapopata shida katika uwanja wa vita, wanasaidiana wakiwa na Matumaini ya kuokoa maisha ya mwenzao, ndivyo Wakristo tunavyokumbushwa leo, kusaidia kubeba mizigo ya wengine na kusaidiana katika kutatua changamoto mbalimbali. Sisi sote tu viungo vya mwili mmoja katika Kanisa la Mungu; kila mmoja wetu ana jukumu muhimu la kutekeleza katika mwili huo. Katika mfano wa Msamaria Mwema, tunaona mtu ambaye pengine alihatarisha hata maisha yake ili kubeba mizigo ya mtu aliyeibiwa na kujeruhiwa na wezi/wanyang’anyi. Msamaria mwema alisaidia kubeba mizigo wa mtu huyo kwa kutunza mahitaji yake ya kimwili, matibabu, kulipia chumba chake na chakula.

Je, ni namna gani sisi tunaweza kubeba mizigo ya wengine nyakati hizi? Wapendwa, ziko namna mbalimbali za kuchukuliana Mizigo, lakini jambo la muhimu kwetu sote ni kudumu katika uhusiano licha ya changamoto zilizopo. Tukidumu katika Uhustiano mzuri, itakuwa ni rahisi kujua mizigo walijonayo wengine. Tutapata nafasi ya kuwasikiliza. Wakati mwingine tumetingwa, kiasi kwamba tunakosa kuwasikiliza wengine, pengine tungewasikiliza kumbe shida yao ilikuwa ndogo tu, ingeisha mapema!

Kubeba mizigo haimaanishi kuwa lazima ubebe wewe mwenyewe. Wakati mwingine unaweza ukawa huna uwezo/nafasi ya kusaidia kubeba mizigo wa mwingine, lakini unaweza ukawa Daraja/kiunganishi ukajua mtu anayeweza kusaidia. Hapo pia utakuwa umefanya kwa sehemu kusaidia kubeba mizigo wa mtu huyo.

Kuna baadhi ya mizigo ambayo watu wanaweza kutusaidia kubeba. Lakini kuna baadhi ya Mizigo ambayo hakuna Mwandamu anaweza kustahimili kwa ajili yetu. Mizigo ya namna hiyo ni lazima tutegemee msaada wa Mungu pekee. Ni lazima twende kwake. **Yesu anasema: Njoni kwangu ninyi nyote mnaolemewa na Mizigo, nami nitawapumzisha (Mt.11:28)**. Kwa hiyo Mizigo ambayo

imetushinda, tunaalikwa twende nayo kwake ili atusadie. Kumbuka Nira huunganisha vitu viwili ili vigebe mzigo pamoja. Sisi nasi tumefungwa nira kwa Mwokozi, ambaye alibeba Mizigo yetu, alibeba mzigo wa Ulimwengu mzima, na hata sasa Yesu yuko pamoja nasi, wakati mwingine anashiriki katika Mizigo tuliyonayo pasipo hata sisi kujuu. Iko shida, kwamba wakati mwingine tunaona mizigo imetuzidi hatutaki kuipeleka kwa Yesu ili atusadie. Inawezekana tunadhani kwamba kwa sababu mizigo hiyo imetushinda, basi ni mikubwa kuliko Yesu. Inawezekana hata mzigo wa janga ambalo lipo sasa, tunadhani ni mkubwa kuliko Yesu. Ukweli ni kwamba hakuna mzigo ambao unamshinda Bwana Yesu. Anasema njooni.....

Ni hakika kwamba wengine wanahitaji msaada wa kifedha ili kusaidia kupunguza mzigo walio nao, lakini wengine wanahitaji maneno ya faraja na kuwatia moyo tu, wengine wanahitaji ushauri wa kiroho tu, wengine unahitaji kuomba pamoja nao ndipo mizigo yao inaisha. Wengine mizigo yao ni upweke, wanahitaji kutembelewa majumbani mwao. Tunapofanya hivyo, tunakuwa miguu na mikono ya Mungu katika kuwasaidia wengine katika nyakati zao za uhitaji. Mungu amechagua kufanya kazi kupitia sisi.

Udugu uliopo kati ya usharika wa **Himmelfahrt** (kupaa) na sharika za **Mwakaleli, Isange** na **Mbigili** au Udugu kati ya Kanisa la Bavaria na Kanisa la Tanzania ambapo ndani yake tunachukuliana Mizigo, ni kusudi la Mungu na ni mfano halisi wa Kuchukuliana Mizigo. Katika Yesu sisi ni Kaka na Dada, tumefanyika familia kubwa ya Mungu, tumeunganishwa pamoja katika ushirika wa pamoja kwa Roho Mtakatifu. Katika Familia hii kubwa ya Mungu tunashiriki imani yetu pamoja wengine, matendo ya upendo na huruma kwa wengine yanafanyika ambayo kwa sehemu ni wonyesho wa Imani yetu katika matendo. Mungu mwenyewe aendelee kuimarisha Udugu huu tuendelee kufanyika Baraka kwa wengine sasa na hata milele.

Na amani ya Mungu ipitayo akili akili zetu zote, iwashifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. Amina.

Mchg. Yusuph Mbago